# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

**AnwaniyaSimu:"UCHUNGUZI"**
**SimuNambari: 2150043 – 6/2150360**
**Fax No: (022) 2150047**
**E-mail:dgeneral@pccb.go.tz**
**Website:www.pccb.go.tz**

**Unapojibutafadhalitaja:**

Mtaa wa mkoani
**S. L. P 273,**
**55103 SUMBAWANGA**
**TANZANIA**

**11/06/2020**

**TAARIFA YA FEDHA ILIYOOKOLEWA NA TAKUKURU MKOA WA RUKWA TSHS 175,983,250/=**

**Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa**

**Wageni waalikwa**

**Mabibi na mabwana Asalaam Aleykum**

Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa , Mbele yako ni walimu wastaafu 39 wa Halmashauri za wilaya za Sumbawanga na Kalambo ambao pia walikuwa wananchama wa CHAUWAMI SACCOS.Vile vile wapo viongozi wa Nkasi Teachers Saccos ambacho pia ni chama cha Akiba na Mikopo cha walimu wanaohudumu katika wilaya ya Nkasi na pia tunao viongozi wa MAKUPA SACCOS NA TUNAE PIA Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya wilaya ya Sumbawanga ambao kwa pamoja wanashiriki katika hafla hii ya urejeshaji wa fedha zilizokuwa zimeppotea katika mikono stahiki na salama.

Mh Mkuu wa Mkoa sehemu ya fedha hizi Tshs 169,828,000/= zitakabidhiwa kwa makundi matatu ya wanufaika kama nitakavyoelezea hapa chini:

I. **SHS. 45,315,000/= ZINAREJESHWA BENKI KUU KATIKA AKAUNTI MAALUM.**

Mh. Mkuu wa Mkoa, moja ya majukumu ya Takukuru ni kukagua miradi ya maendeleo na katika kutktltza jukumu hili katika Mradi wa Umwagiliaji wa Katongolo kule wilayani Nkasi ilibainika kuwa Mkandarasi ambaye ni Kampuni ya Girson Investments Ltd alikuwa amelipwa fedha nyingi kuliko kazi alizokuwa ametekeleza.Kipaumbele kwa serikali ni kuhakikisha kuwa fedha hii inarejeshwa Serikalini wakati hatua nyingine za kisheria zikiendelea.Mpaka sasa Mkandarasi amekwisharejesha Tshs. 45,000,000/= ambazo zinazorejeshwa katika Akaunti

maalum iliyoko Benki Kuu ya Tanzania . Tshs. 315,000/= ni fedha ambazo zilirejeshwa na Afisa Uhamiaji wilaya ya Nkasi baada ya TAKUKURU kubaini kuwa Mtumishi huyo alipokea kiasi hicho cha fedha kutoka kwa Wahamiaji wa nchi jirani ambao walikuwa wanasafiri kwa basi kupitia nchini mwetu kwenda nchi za kusini mwa Afrika wakiwa na vibali vyote na kueleza kuwa alipokea kama zawadi, pamoja na kuchukuliwa hatua za kinidhamu pia alitakiwa kurejesha fedha hii ambayo pia inaingizwa katika akaunti maalum ya Benki Kuu..

**II. SHS. 96,456,250/= ZINAREJESHWA KWA WANACHAMA WA SACCOS MBALIMBALI MKOANI RUKWA.**

Mh. Mkuu wa Mkoa kati ya fedha hizo kiasi cha Tshs. 56,700,000/= ni fedha wanayorejeshewa Walimu Wastaafu 39 wa SACCOS ya CHAUWAMI ambayo inahusisha walimu wa Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga na Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo.CHAUWAMI Iliundwa kabla ya wilaya ya kalambo haijaanzishwa.Walimu hawa walikuja Takukuru na kulalamika kuwa tangu walipostaafu viongozi wa chama hiki hawajawalipa Amana zao na hawana dalili za kuwalipa na wamefuatilia kwa vipindi vya miaka mmoja hadi minne.

Katika uchunguzi tulioufanywa tubaini kuwa uongozi wa SACCOS hiyo ulitumia AKIBA na HISA za Wanachama wake zote kinyume na Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013.Fedha hizi tuliwabana na wamezirejesha zote na leo hii tutakuomba uzikabidhi kwa walimu hawa wanyonge.

Mh. Mkuu wa Mkoa katika fungu hili kuna Tshs. 39,756,250/= ambazo tutaomba uwakabidhi viongozi wa Nkasi Teachers SACCOS ambazo uongozi wa awali wa SACCOS hiyo uliandaa nyaraka na kuwakopesha watu wasio wanachama kinyume na Sheria ya Vyama vya Ushirika Namba 6 ya mwaka 2013. Uchunguzi huu ulitokana na taarifa ya COASCO ambayo waziri wa Kilimo alimkabidhi Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU kwa ajili ya kuifanyia kazi.Fedha hizi zimerejeshwa na leo tutaomba uwakabidhi viongozi wa Nkasi Teachers Saccos na zitaingizwa katika akaunti ya Chama leo.

Mh Mkuu wa Mkoa Tshs. 1,345,000/= ni fedha za SACCOS ya MAKUPA iliyopo Wilayani Nkasi ambazo ni fedha zilizokopeshwa kwa wanachama lakini wakagoma kuzirejesha kwenye SACCOS yao kwa mujibu wa masharti ya muda wa kufanya Marejesho ya Mikopo yao, na hizi pia tutaomba uwakabidhi viongozi wa Saccos hii.

### III. SHS. 34,212,000/= ZINAREJESHWA HALMASHAURI YA WILAYA YA SUMBAWANGA KUTOKA KWA "DEFAULTERS"

Mh. Mkuu wa Mkoa, mara kadhaa Takukuru tumeshiriki katika kusaidia Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga kukusanya fedha ambazo ama zilikuwa zimepotea au zilikuwa hazijawasilishwa na kuingizwa katika mfumo na katika akaunti za Halmashauri kama taratibu za fedha za Serikali za Mitaa zinavyoelekeza. Mwaka 2019 ulituagiza na tulikusanya zaidi ya Tshs 325,000,000/= Tarehe 08.06.2020 tuilipokea taarifa ya "Defaulters" kutoka kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga baada ya yeye kuagizwa na kikao cha Baraza la Madiwani cha tarehe 06.06.2020 kuiomba TAKUKURU iwasaidie kukusanya Madeni sugu kutoka kwa baadhi ya Watendeji wa Kata na Vijiji katika Halmashauri hiyo. Kwa kipindi cha siku mbili TAKUKURU imefanikiwa kukusanya jumla ya Tshs. 34,212,000/= ambazo leo tutaomba pia uzikabidhi kwa Mkurugenzi wa Halmashauri husika na zoezi la ukusanyaji linaendelea .

Mh. Mkuu wa Mkoa kwa maelezo hayo, Nakuomba sasa nikukaribishe ili utpe nasaha zako na hatimae ukabidhi fedha hizi kwa makundi mbali mbali kama tutakavyokuongoza.

Naomba kuwasilisha

Hamza Mwenda

**MKUU WA TAKUKURU (M)**

**RUKWA**